**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Uzinduzi wa Kamati ya Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani**

**Kuimarisha Juhudi za Utetezi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania**

Leo, tarehe 10 Juni 2024, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unayofuraha kutangaza kamati yake iliyozinduliwa tarehe 6//6/2024 kwa ajilii ya kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za ndani zitakazo saidia Mashirika wadau wa Haki za binadamu hapa nchini Tanzania. Kamati hiyo inaundwa na wakurugenzi 27 wa taasisi (Wanachama wa THRDC) zinazotetea haki za binadamu kwa lengo la kuimarisha utetezi na ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania. Majina ya wajumbe wa kamati yameorodheshwa mwishoni mwa taarifa hii. Kamati hii itafanya kazi chini ya sekretariat ya THRDC.

THRDC yenye wanachama zaidi ya 300 nchini, inathamini kazi ya utetezi wa haki za binadamu inayofanywa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na mashirika ya Haki za Binadamu ya ndani, kikanda na kimataifa; watetezi binafsi; wadau wa maendeleo; Serikali ; Umoja wa Africa na Umoja wa Mataifa. Moja ya majukumu ya msingi ya THRDC ni kuhakikisha watetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania wanakuwa na uwezo wa kifedha ili kufanya kwa ufanisi shughuli za utetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania. Mashirika mengi ya watetezi wa haki za binadamu yamekuwa yakifanya kazi za utetezi ili hali yakiwa na changamoto za upungufu wa rasilimali fedha.

Sote tunajua kuwa ufadhili wa ndani kwa ajili ya mipango ya utetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania unakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa makampuni juu ya majukumu ya taasisi za utetezi wa haki za binadamu, ukosefu au utaratibu hafifu wa ufadhili wa wazi kutoka kwa wafanyabiashara na changamoto ya ufahamu kwa ujumla kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Kwa sasa, takriban asilimia tisini ya shughuli za utetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania zinategemea ufadhili kutoka nje, huku asilimia kumi tu ikitokana na kujitolea kwa wadau wa ndani na usaidizi wa makampuni. Hata hivyo, mwelekeo wa ufadhili wa kimataifa unaonyesha kuna mabadiliko katika vipambele vya wafadhili mbali na miradi ya haki za binadamu kutoka nchi za

nje ya Tanzania. Katika kukabiliana na hali hii, kamati itaongeza juhudi za kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za ndani, tukiamini kuwa umiliki wa ndani na uhamasishaji wa rasilimali ni muhimu kwa uendelevu na mustakabali wa shughuli za haki za binadamu. Kamati inalenga kufanya kazi kwa karibu na wafanyabiashara/makampuni ili kuunganisha mikakati ya Uwajibikaji kwa Jamii (*Corporate Social Responsibility*) ambayo inalingana na mipango ya haki za binadamu.

Mashirika ya haki za binadamu yana mchango mkubwa katika kukuza na kutetea haki za binadamu nchini Tanzania katika ngazi mbalimbali. Wengi wao hufanya kazi kwa hiari bila kupata rasilimali fedha kutoka kwa wafadhili wa ndani au washirika wa nje. Mashirika ya haki za binadamu yanafanya kazi katika afua mbalimbali za haki za binadamu kama vile haki za wanawake, haki za watoto, huduma za msaada wa kisheria, mabadiliko ya hali ya tabia ya nchi nchi, haki za watu wenye ulemavu, mabadiliko ya sheria, uwajibikaji, haki za mazingira, utoaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, afya n.k. Kazi za mashirika ya utetezi wa Haki za binadamu yameleta mchango mkubwa wa maendeleo katika nchi yetu.

Kwa miaka mingi sasa, licha ya kazi nzuri iliyofanywa na mashirika ya haki za binadamu, hakujawa na uratibu wowote unaofaa kuhusu jinsi jamii ya wafanyabiashara inaweza kuchangia kazi za haki za binadamu kwa ujumla. Ni kutokana na hali hii Mtandao umeamua kuunda kamati ya kuweka utaratibu mzuri wa jinsi gani Jamii ya Wafanyabiashara na makampuni binafsi wanaweza changia kazi za utetezi hapa nchini.

Madhumuni ya jumla ya Kamati ya Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani ni kutoa mwongozo na kuunga mkono juhudi za mashirika ya utetezi wa haki za binadamu katika kukusanya rasilimali, ikiwa ni pamoja na kutambua na kutekeleza mipango ya ubunifu ya kifedha kwa kuzingatia vyanzo vya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mipango yao ya uendeshaji na uendelevu kifedha. Kamati hiyo imepewa jukumu la kutanua wigo wa ufadhili nchini Tanzania kwa kuandaa mkakati wa kitaifa wa kushawishi sekta binafsi kusaidia mashirika yote ya haki za binadamu hapa nchini yakiwemo mashirika wanachama na yasiyo wanachama wa THRDC.

Kwa hiyo tunakaribisha jamii ya sekta binafsi nchini Tanzania kuunga mkono hatua hii kwa sababu faida za kusaidia shughuli za haki za binadamu ni nyingi. Pia tunatoa wito kwa wanachama wa Mtandao wa THRDC na taasisi nyingine za haki za binadamu nchini Tanzania kuunga mkono mpango huu wa uendelevu wa kazi za haki za binadamu nchini Tanzania.

**<u>Imetolewa Leo Tarehe 10/June/2024 na</u>**

**Onesmo Kasale Olengurumwa**

**Mratibu Taifa-THRDC .**

**ORODHA YA WANAKAMATI**

1) Dr John Kalage, Mkurugenzi HakiElimu – Mwenyekiti wa Kamati

2) Dr. Mzuri Issa Ali, Mkurugenzi Tanzania Media Women Association (TAMWA) Zanzibar – Mwenyekiti Mwenza wa Kamati

3)Wakili Onesmo Olengurumwa, Mratibu Kitaifa Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC) – Katibu wa Kamati

4) Bw. Clemence Mwombeki, Mkurugenzi Door of Hope to Women and Youth in Tanzania - Mjumbe wa Kamati

5) Bw. Abdalla Abeid, Mkurugenzi Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization (ZAFAYCO) - Mjumbe wa Kamati

6) Bw. Suleiman Mujuni Baitani, Zanzibar Coordinator THRDC ZANZIBAR - Mjumbe wa Kamati

7) Dr. Anna Henga, Mkurugenzi Legal and Human Rights Center (LHRC) - Mjumbe wa Kamati

8) Mhe. Fatma Toufiq Mkurugenzi Women Wake Up (WOWAP) - Mjumbe wa Kamati

9) Bi. Justa Mwaituka, Mkurugenzi Kiota Womens Health and Development (KIWOHEDE)- Mjumbe wa Kamati

10) Bw. Samuel Nsokolo, Mkurugenzi Nguruka Development Agency (NDA) - Mjumbe wa Kamati

11) Bi. Editrudith Lukanga, Mkurugenzi Environmental Management and Economic Development Organization (EMEDO) - Mjumbe wa Kamati

12) Bi. Sophia Leghela, Mkurugenzi Zanzibar Child Rights Forum (ZCRF) - Mjumbe wa Kamati

13) Bi. Angela Benedict, Mkurugenzi Wote Sawa - Mjumbe wa Kamati

14) Bi. Tike Mwambipile, Mkurugenzi Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA) - Mjumbe wa Kamati

15) Bw. Bakar Hamad, Mkurugenzi Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA) - Mjumbe wa Kamati

16) Wakili Jamila Mahmoud Juma, Jamila Mahmoud Juma Mkurugenzi Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA) - Mjumbe wa Kamati

17) Bw. Alawy B. Hamad, Mkurugenzi The Popular Inspiring and Relief Organization (PIRO) - Mjumbe wa Kamati

18) Bw. Zacharia Faustin, Mkurugenzi Tanzania Natural Resources Forum (TNRF) - Mjumbe wa Kamati

19) Bi. Rose Reuben, Mkurugenzi Tanzania Media Women Association (TAMWA) - Mjumbe wa Kamati

20) Bw. Jonas Lubago, Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) - Mjumbe wa Kamati

21) Bw. Esaya Yusuf, Mkurugenzi Sustainable for Environmental; Climatic Change Association (SECCA) - Mjumbe wa Kamati

22) Bi. Aginatha Rutazaa, Mkurugenzi Tusonge Community Development Organization (TUSONGE CDO) - Mjumbe wa Kamati

23) Bi. Herrieth Mkaanga, Mkurugenzi My Health Foundation - Mjumbe wa Kamati

24) Bw. Paul Ole Kurupash, Mkurugenzi Namnyaki Girls and Women Organization (NAMGWO) - Mjumbe wa Kamati

25) Bw. Gerald Ng'ong'a, Mkurugenzi Rafiki SDO - Mjumbe wa Kamati

26) Bi. Hilda Stuart Dadu, Mratibu Kitaifa - Coalition for Women Human Rights Defenders (CWHRD) - Mjumbe wa Kamati

27) Bi. Maanda Ngoitiko, Mkurugenzi Pastoralist Women Council (PWC) - Mjumbe wa Kamati